



FAMILY BENEVOLENCE FUND (FBF)

*MFUKO WA
MASAIDIANO WA
FAMILY (MMF)*

ffamily

Kusudi:

Mpango huu wa mfuko umeundwa kwa ajili ya kuwasaidia wanachama wa FAMILY kukabiliana na mzigo wa kifedha unaotokana na matukio ya kijamii (*kufiwa, harusi, send-off, ajali, majanga ya asili, magonjwa ya muda mrefu yasiyo ya kuambukizwa*).

Huenda usigharamie gharama zote lakini umekusudia kupunguza mzigo wa kifedha kwa mwanafamilia.

VIFUNGU VYA MUHTASARI

01

Wigo wa Mpango:

Wanafamilia watakaohudumiwa na mfuko: Mwanachama wa **FAMILY (Mwanafamilia), mwenzi, watoto, na wazazi tu.**

02

Usajili:

Ada ya usajili ya mara moja ambayo haiwezi kurejeshwa ni Tshs 200,000 kwa kila mwanachama. Kila mwanachama atatakiwa kujisajili kwa kutumia fomu iliyoambatanishwa. Kwa wanandoa, kila mwanandoa atatakiwa kujiandikisha kama **mwanachama binafsi** na kila mmoja atalipa Tshs 200,000 kwa mwaka, kiasi ambacho kitatolewa si zaidi ya mara 4 katika mwaka husika (kila miezi mitatu angalau elf 50).

03

Kila mwaka

mwanachama atatakiwa kuchangia 50,000 kwa ajili ya kutunisha mfuko wa familia.

04

Msaada wa Kifedha:

Kiasi cha sasa cha kulipwa kwa mwanachama endapo atapatwa na mojawapo ya mambo tajwa hapo juu atachangiwa Tshs 2,500,000 kutoka kwenye mfuko, na kwa wategemezi mwanachama atachangiwa 1,500,000.

05

Mchango wa Kutunisha Mfuko:

Kufuatia utoaji wa fedha kwa mwanachama, mfuko utakuwa ukijazwa kwa mchango wa pamoja ili kufidia jumla ya fedha zilizotolewa kwa wanachama kwa mwaka uliopita. Mchango huu utakamilika ndani ya miezi mitatu (siku 90).

06

Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha katika Mfuko:

40% ya mfuko ifanyiwe uwekezaji mf, ununuzi wa bond za serikali, 40% itumike kwa ajili ya kazi ya Mungu na 20% ibaki kama akiba ya mfuko.

TARATIBU ZA KUTUNISHA MFUKO BAADA YA PESA KUTOLEWA KWA MWANACHAMA

i.

Iwapo mwanachama hatatoa mchango ndani ya muda husika (siku 90 za kwanza), basi atasimamishwa hapo hapo kwa siku 30 na **HATATAKIWA** kupokea fedha yoyote endapo atapata mambo tajwa hapo juu ndani ya hizo siku 30. Ikiwa mwanachama aliyesimamishwa atalipa **deni** lake kikamilifu ndani ya siku 30 za kusimamishwa, atarejeshwa kwenye mfuko baada ya siku 30 tangu tarehe ya malipo ya fedha ilipotolewa.

ii.

Ikiwa mwanachama hatachangia kufikia tarehe ya mwisho iliyotajwa (siku 90), na bado hajachangia ndani ya siku 30 baada ya tarehe ya mwisho uanachama wake utasitishwa. Na kama atapenda kurudi basi atafuata utaratibu wa usajili kama mwanachama mpya.

iii.

Mwanachama atahesabiwa kuwa anakidhi vigezo vya kuchangiwa endapo amechangia angalau asilimia 75 ya ada ya kiingilio, mchango wa 50,000 wa kutunisha mfuko kila mwaka pamoja na kurudisha kiasi kilichochangiwa kwa mwaka uliopita (rejea na 3 na 5 hapo juu).

Baada ya mfuko kuanza kufanya kazi, usajili wa wanachama wanya utafanyika wakati wowote. Baada ya mwanachama kukidhi vigezo vya usajili, mwanachama mpya atasubiri muda ya siku 90 kabla uanachama wake kuwa HAI na kuanza kupokea fedha kutoka kwenye mfuko.

Sheria na kanuni za mpango huu zinaweza kubadilika kulingana na wakati na uanachama wa mfuko kukua ili kuruhusu wanachama kutumia kikamilifu manufaa yanayotolewa na mpango huu. Uongozi wa FAMILY kwa kushirikiana na wanachama unaweza kufanya mabadiliko inapobidi.
